

SEHEMU YA PILI

MATAYARISHO YETU KIBINAFSI

LENGO: *KUTEKELEZA MAHITAJI BINAFSI YA MUNGU MAISHANI MWETU YATAKAYOTOA NGUVU KATIKA SALA ZETU NA KUWAFANYA WAPOTEVU KUITIKIA USHUHUDA WETU KWAO.*

1. BIBLIA HUFUNDISHA DHAHIRI KWAMBA MITINDO YA MAISHA YETU BINAFSI ITAAMUA IKIWA MUNGU ATAYAJIBU MAOMBI YETU AU LA.

A. Mungu atatupatia yale tunayomwomba KWA SABABU ya mtindo wa maisha yetu unaotii amri zake.

“Na twaweza kupokea kwa cho chote tuombacho, maana twazitii amri zake na kufanya yale yampendezayo.” 1 Yohana 3:22.

1. Maneno ‘Weka’ na ‘Fanya’ yako katika ngeli ya ‘sasa’ iendeleayo katika lugha ya kigriki, maana yake kuendelea kumtii na kumpendeza Mungu bila kusita.
2. Hili silo jambo la kufanywa kwa kushtukia tu wakati mmoja, yale Mungu atutarajia tufanye.

B. Katika Yohana 15:7, Yesu alisema, neno ‘ikiwa’ liko mara mbili ambazo ndizo zitakazoamua kutekelezwa na Mungu ahadi ya nguvu za sala.

“Ikiwa mtakaa ndani yangu na (ikiwa) maneno yangu yakikaa ndani yenu, basi ombeni mtakacho, nanyi mtapewa.”

1. Hii ndiyo ahadi thabiti zaidi ya kuombea katika agano jipya.
2. Lakini, Yesu alitoa ahadi hiyo ikiwa tu tutatekeleza matakwa yake ya ‘ikiwa’ mbili maishani mwetu.
 - a. *“Kuishi ndani ya Yesu”* kwamaanisha kuwa sehemu ya mwili wake, kupitia uokovu, na kisha kupata riziki na nguvu zetu za kila siku hutoka kwake.
 - b. *“Maneno yake yakaa ndani yetu”* - maana yake ni - lazima tuishi na kutii maneno yake yote, miongoni mwayo yakiwa:
 1. Yote ambayo Yesu alinena duniani . (Yohana 14:25)
 2. Kuwasomea wafuasi wake maandiko matakatifu kutoka agano la kale. (Luka 24:27,45)
 3. Maneno yake ambayo Roho Mtakatifu aliwaambia wafuasi wake wayaandike. (Yohana 14:25-26).
 4. Maneno ambayo Yesu alimwambia Yohana baada ya kurudi mbinguni. (Ufunuo 2 na 3)
3. Haya ndiyo maneno yote ya Yesu katika Biblia ambayo alisema lazima tuyatii ili tuweze kupata majibu kwa sala zetu.

II. BIBLIA HUTOA MASHARTI GANI ILI TUWEZE KUPATA NGUVU ZA MUNGU KATIKA SALA NA USHUHUDA?

A. **Lazima tunjue Yesu binafsi.**

1. *“Kuishi katika Yesu”* ili kupata uwezo wa maombi katika Yohana 15:7 hakuwezekani bila kumjua binafsi kuwa mwokozi na Bwana.
2. Hakuna ahadi katika agano jipya ya kupata uwezo kutokana na kuwaombea wale wasiomwamini Yesu.
3. Fursa ya enzi ya agano jipya ya kuomba *‘katika jina la Yesu’* (Yohana 16: 24) ilipewa tu wale waliokuwa wafuasi wa Yesu.

Chunguza moyo wako: HAKIKISHA WAMJUA YESU BINAFSI KABLA HUJARIBU KUWAOMBEA WENGINE WAOKOKE. IKIWA SIVYO OMBA UKITUMIA MAAGIZOKATIKA sehemu ya 6, ukurasa wa 28 na 29.

B. Hakupasi kuwepo na dhambi inayojulikana ambayo haijatubiwa katika maisha ya mwombaji.

1. Basi mtu ambaye hafanyi lile jambo jema (kutoka Biblia) analojua kwamba apaswa kulifanya, anatenda dhambi. Yakobo 4:17.
2. Zipo aina mbili za dhambi katika Biblia - Dhambi ya umoja na dhambi ya wingi.
 - a. Dhambi ya umoja ni ile hali ya dhambi ambamo sote tulizaliwa nayo (Yohana 3:18 na Waroma 5:18)
 1. Kwa Yesu, ulimwengu, daima ulikuwa wale ambao hawajamkubali kuwa mwokozi. *"Naye atakapokuja (Roho mtakatifu) atawathibitisha walimwengu kwamba wamekosea kuhusu dhambi, uadilifu, na hukumu ya Mungu. Wamekosea kwa sababu hawaniamini,"* Yohana 16:8 - 9.
 2. Yesu alikuja akihubiri *"Tubuni na mwamini."* (Mariko 1:15)

Chunguza moyo wako: Hakikisha kwamba ulipomkubali Yesu kuwa mwokozi wako, hukuamini tu, bali ulitubu dhambi zako.

- b. Dhambi za wingi ni dhambi ambazo twazifanya baada ya kuwa wakristo.
 - (1) Yesu aliwafundisha wafuasi wake (pekee) sala ya Bwana katika Matayo 6:9-12 Kuomba hivi:
"Baba yetu uliye mbinguni utusamehe MAKOSA YETU" (Makosa, maana yake ni dhambi.)
 2. Mtume Yohana aliwaandikia tu wakristo kitabu cha kwanza cha Yohana na akasema katika 1:9 *"Tukitubu dhambi zetu"* Mungu atatusamehe na kututakasa.
 3. Petero alikuwa akiwaandikia wakristo aliposema katika 1 Petero 3:12 *"Macho ya Mungu huwatazama kwa wema watu waadilifu na kusikiza sala zao, lakini huwapa kisogo watendao maovu."*
 4. Katika 1 Yohana 3:22, *"Kutotii"* na *"Kutotenda yasiyompendeza Mungu"* ni dhambi.
 5. Ni sala za WATU WEMA katika Yakobo 5:16 zilizo na *"nguvu na hutenda mengi."*
 6. Soma maneno ya Yesu **"Tubuni"** katika ufunuo sura za 2 an 3 aliyoyapelekea makanisa yake ya kikristo (sisi) baada ya kurudi mbinguni. (Soma pia 11 Mambo ya nyakati 7:14, Zaburi 66:18, Zaburi 51:10-13 na Zaburi 24:3-5)
 7. Ufufuo wote, tangu nyakati za Yesu hadi sasa ulianza wakati wakristo wachache walipomwamini Mungu kamili (11Mambo ya nyakati 7:14 na Petero 4:17)

Chunguza moyo wako: UNAPOUNGAMA DHAMBI ZAKO BAADA YA SEHEMU HII, KUMBUKA MAHITAJI HAYA.

C. Lazima tusamehe tunavyosamehewa.

1. Yesu katika sala yake ya Bwana, aliweka sharti kwa msamaha wa Mungu kwa dhambi za wakristo - nasi tuwasamehe wengine.
"Utusamehe makosa yetu kama tunavyowasamehe waliotukosea," Matayo 6:12.

2. Punde tu baada ya sala ya Bwana, Yesu aliongeza kwamba IKIWA sisi (Wakristo twawasamehe wengine, Mungu naye atatusamehe, lakini tusipowasamehe, Mungu hatatusamehe dhambi zetu tulizotenda tukiwa wakristo. (Matayo 6: 14-15) (Hii haiwahusu wasio wakristo kusamehewa wanapomkubali Yesu kuwa mwokozi wao).
3. Yesu aliunganisha kupokea kutokana na kuomba kwa imani katika Mariko 11:24 na 'na' katika Mariko 11:25 - kwamba tunaposimama tukiomba, yatupasa tusamehe, kwa sababu tusipofanya hivyo, Mungu naye hawezi kutusamehe.
4. Kwa hivyo tusiposamehe, dhambi zetu tulizozitenda (ingawa tumeziungama, hazitasamehewa na Baba ikiwa hatutawasamehe wale watukoseao; hivyo basi sala zetu hazitajibiwa na Mungu.

Chunguza moyo wako: HAKIKISHA KWAMBA HUKATAI KUMSAMEHE YE YOTE KWA MAKOSA-ALIYOKUFANYIA.

D. Omba katika imani.

1. Imani ni muhimu ili kumpendeza Mungu, hivyo basi tutapokea majibu YAKE kwa maombi yetu. Waebrania 11: 6.
2. Imani hii katika Mungu haihusiki na anavyofikiri mwombaji, lakini vile neno la Mungu lisemavyo ukiamini kwamba ndiye, na pia kuamini kwamba ni mtunzaji wa wale wanaomuhitaji kwa bidii.

Chunguza moyo wako: MWOMBE MUNGU AONGEZE IMANI YAKO NA AKUSAIDIE UAMINI KATIKA VITU UNAVYOOMBA.

E. Lazima tuombe katika mapenzi ya Mungu.

1. Ijapokuwa Biblia wakati mwingine huonekana kama yatuambia kwamba twaweza kuomba chochote tutakacho, Yesu alipofundisha jinsi ya kuomba katika sala yake ya Bwana, Alisema lazima tuombe "*Baba utakalo lifanyike.*"
2. Yesu alikuwa kielelezo kwetu kwa kujitolea kwa matakwa ya Baba yake katika shamba la Getisemani kabla ya kwenda msalabani. Luka 22:42
3. Tunapojitoa kwa matakwa ya Baba twajileta wenyewe na matakwa yetu, kulingana na yake.
 - a. Kisha twaomba chochote tanachokihitaji, kwa sababu hatuhitaji chochote ambacho hakilingani na matakwa ya Baba.
 - b. Hii ni pamoja na kujitoa kwa matakwa ya Mungu katika maisha yetu binafsi na katika maombi yetu.
 - c. HATA HIVYO, KAMWE USIMUULIZE MUNGU IKIWA NI MATAKWA YAKE KWETU KUMWOMBEA MTU ILI AOKOLEWE, KWA KUWA 2 Petero 3:9 yatuambia kwamba Bwana hapendi yeyote apotee, bali huwavuta wote wapate kutubu.

Chunguza moyo wako: HAKIKISHA KWAMBA HUKAIDI MATAKWA YA MUNGU MAISHANI MWAKO AU KILE UNACHOOMBEA. IKIWA WAFANYA HIVYO, WACHA YOTE KWA MATAKWA YA MUNGU.

F. **Lazima tuendeleo kuomba kila siku.**

1. Yesu alituumuru tuombe katika mahali faragha badala ya kuonekana na kusikika na watu. Matayo 6:5-6.
2. Ni katika wakati huu wa unyenyekevu mkuu ambapo:
 - a. Twamkaribieni Mungu, naye atakuja karibu nasi. (Yakobo 4:8)
 - b. Twatubu dhambi. (Yohana 1:8-9)

- c. Twamwabudu na kumsifu Mungu (Zaburi 100)
 - d. Twasamehe wengine (Waefeso 4:32)
 - e. Twamsikiza Mungu (Mhubiri 5:1-2)
 - f. Twajitoa kwa matakwa ya Mungu maishani mwetu. (Matayo 6:10)
 - g. Twapata ushindi juu ya shetani (Waefeso 6:12-13).
 - h. Twabadilishana mapenzi yetu na Mungu. (Mariko 12: 30)
 - i. Twapata uwezo kwa maisha yetu na kwa kazi ya Mungu. (Matendo 1:8)
 - j. Twawaomba wengine kila siku (Waefeso 6:18)
3. Nguvu za sala zetu za hadhara katika vikundi vya watu watatu, makundi, na sala za wengi, hutegemea thamani na kiasi cha sala zetu za faragha. (II Mambo ya nyakati 7:14)

Chunguza moyo wako: MWAHIDI MUNGU KWAMBA UTALINDA NA KUTHAMINI SALA ZAKO ZA KILA SIKU.)

G. Lazima tuombe bila kukoma.

1. Tuondokapo kutoka chumba chetu cha maombi ya kila siku, tusishindike mlango tukimwahidi Mungu kwamba tutakutana naye tena kesho.
2. La, tuendee kuwasiliana na Mungu kwa saa 24 kila siku, hata tuwe tayari kuomba tunapokosa usingizi usiku. (I Watesalonike 5:17, Luka 18:1)
3. Roho mtakatifu aonekana kuwashawishi wapotevu kulingana na jinsi tunavyowaomba.

Chunguza moyo wake: MWOMBE MUNGU AKUJAZE NA HAMU NA UWEZO WA KUENDELEA KUSALI

H. Lazima tusali kwa kusudi maalum.

1. Yakobo 4:3 atuambia kwamba tunapomba, hatupati kwa sababu tunaomba kwa nia mbaya.
2. Sababu yetu ya kuwaomba wapotevu yapasa iwe kwamba twawapenda, na twaamini kwamba wamelaaniwa milele wasipompokea Yesu kuwa mwokozi wao - si kwa mafanikio yetu na fahari zetu binafsi.

Chunguza moyo wako: CHUNGUZA SALA ZAKO ZA HIVI KARIBUNI KUJUA NI KWA NINI ULITAKA YALÉ ULIYOOMBA, HATA ROHO ZILIZOPOTEA.

1. Lazima tumkaidi shetani.

1. Kwa kuwa kuwaomba na kuwaokoa wapotevu ni kuwakomboa wafungwa kutokana na utawala wa shetani (Wakolosai 1:13, lazima tutambue mbinu zake za uongo, kisha tumkaidi kikamilifu (Yakobo 4:7)
2. Lazima tilidai jina la Yesu (Wafilipi 2:9-11 na Wakolosai 1:15-17) na DAMU YA YESU kumpinga shetani. (Ufunuo 12:9-11 na 5:8-9) kwa kuwa ingawa hatuna uwezo wa kupigana, shetani hawezi kustahimili nguvu za jina na damu ya Yesu.

Chunguza moyo wako: JIZOESHE KWA MAKINI KUPIGANA NA SHETANI ANAPOJARIBU KUKUZUIA.

III. MUNGU HUTEKELEZA WAJIBU GANI KATIKA MATAYARISHO HAYA YA KIBINAFSI KWA MAOMBI KAMILI YA KUENEZA INJILI?

- A. Mungu ajua kwamba mwanadamu hawezi kutosheleza mahitaji haya yote bila msaada, kwa hivyo usijaribu.
- B. Lakini aliahidi kwamba yeye mwenyewe ndiye atakayefanya hivyo ndani yetu.
"Kwani Mungu ndiye afanyaye kazi daima ndani yenu na kuwapeni uwezo wa kutaka

na kutekeleza mambo yanayopatana na mpango wake mwenyewe. Wafilipi 2:13.

1. Kwa kuwa Mungu alitupatia mahitaji haya yote katika neno lake takatifu, Biblia, twajua tu kusudio lake.
 2. Basi, twajua kwamba atafanya hivyo ndani yetu licha (sisi) kuwa hafifu.
- C. Roho mtakatifu wa Mungu huzua hamu ndani yetu, ya kuishi kitakatifu, ana hamu, na anangojea kutusaidia.
- D. Yesu aliye mbinguni anatuomba sasa (Waroma 8:34. Wahibrania 7:24-25)

MAZOEZI

Soma kwa makini na maombi, orodha ya dhambi iliyomo humu, ukimwomba Mungu akuhukumu kwa dhambi yo yote ambayo ingali maishani mwako au haijaungamwa. Tafakari juu ya mahitaji ya kibinafsi na kibiblia katika somo hili kwa uwezo wa sala ili uweze kutubu kama dhambi, chochote kinachokosekana maishani mwako.

Mwombe Mungu akukumbushe dhambi zo zote ambazo hazijaungamwa. Kisha ungoje, ukiwa mnyamavu, akukumbushe.

SALA YAKO

1. *Ukiwa peke yako*, ungama katika sala, kila dhambi ambayo Mungu amekukumbusha kupitia orodha hiyo, au kwa kusoma Biblia.
2. *Ukiwa na wengine*, unda vikundi vidogo vya watu wapatao wanne kila kimoja. Na kwa sauti kubwa, omba “Baba, nisamehe” Kisha taja kila dhambi wataka isamehewe, endelea mpaka zote ziishe.

Kuomba pamoja kwawezesha kuwasaidia wale kati yenu walio na haya, waoga, na waombaji wapya jinsi ya kusali, na husaidia wenye kiburi kuwa waaminifu. Lakini kama nyote katika kikundi chako ni waombaji wkomavu, ungameni dhambi zenu kwa zamu.

Amua ikiwa wataka kutaja kwa sauti kubwa au la, dhambi ambayo yapasa kuwa kati yako na Mungu pekee. Mwombe Mungu akusamehe dhambi unayofikiria.

3. Kubali msamaha kutokana na Neno la Mungu. I Yohana 1: 8-9
4. Kumbuka kwamba ni dhambi zinazojulikana ndizo tunazozitubu kupata uwezo wa Mungu katika sala. Usimtarajie Mungu kukufunulia wakati mmoja kila dhambi uliyofanya, lakini uwe tayari kuungama dhambi zaidi, jinsi anavyoendelea kukufunulia.

Kwa maelezo kamili kuhusu mahitaji haya, soma kitabu kilitwacho “*Nini hutokea wanawake wanapomba.*” Kilichoandikwa na Evelyne Christenson.

ORODHA YA DHAMBI YA KUSOMWA KABLA YA KUUNGAMA DHAMBI KATIKA SALA.

(Tumia utaratibu wako mwenyewe kufanya hivyo)

Kila jibu 'ndio' ni dhambi katika maisha yako na huhitaji kuungamwa. "Basi mtu ambaye hafanyi lile jambo jema analojua kwamba apaswa kulifanya, anatenda dhambi." (Yakobo 4:17) (MTAJO KATIKA KURASA HIZI MBILI WATOKA KJV)

1. Watesalonike 5:18 *"Muwe na shukrani katika kila hali. Hayo ndiyo anayotaka Mungu kwenu katika kuungama kwenu na Kristo yesu.*
Una wasi wasi kuhusu chochote? Umekosa kumshukuru Mungu kwa kila kitu, vibaya na vizuri? Wapuuza kushukuru kabla ya kula?
2. Waefeso 3:20 *"Kwake yeye ambaye kwa nguvu zake ifanyayo kazi ndani yetu, aweza kufanya mambo makuu zaidi ya yale tuwezayo kuomba au kufikiria."*
Wakosa kujaribu kufanya mambo kwa niaba ya Mungu kwa sababu huna kipawa cha kutosha? Je, wakosa kujaribu kumhudumia Mungu kutokana na fikira kwamba u-duni? Ni lini unapomkamilishia Kristo chochote? Je, wakosa kumtukua kikamilifu?
3. Matendo 1:8 *"Lakini wakati Roho Mtakatifu atakapowashukieni ninyi, mtajazwa nguvu na mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, katika nchi yote ya Yudea na Samaria, hata kwenye mipaka yote ya dunia."*
Je, umeshindwa kuwa shahidi wa maisha yako kwa Kristo? Umewahi kuhisi kwamba yatosha kuuacha Ukristo wako na usishuhudie kwa kinywa chako kwa wapotevu?
4. Waroma 12:3 *"Kutokana na neema aliyonijalia Mungu, nawaambieni ninyi nyote: Msijione kuwa ni kitu zaidi ya mnavyopasa kuwa."*
Wajivunia mafanikio yako, vipawa vyako, jamaa yako? Wafikiria kwamba watu wengine hawawezi kuwa bora kuliko wewe, muhimu kukuliko katika mwili wa Kristo? Je, huwa wasistiza haki zako binafsi? Wafikiri kwamba ukiwa mkristo waendelea vizuri sana? Je, wamwasi Mungu anapojaribu kukubadilisha?
5. Waefeso 4:31 *"Basi achaneni na uhasama, chuki, hasira, kelele matusi! Achaneni na kila uovu."*
Je, walalamika, kuwapata wenzako makosa, bishana? Wawahusudu wakristo wa kundi jingine kwa sababu hawakubaliani nawe kuhusu mambo yote? Waongea vibaya kuwahusu watu ambao hawako nawe? Wajikasirikia? Wawakasirikia wengine? Mungu?
6. 1 Wakorintho 6:19 *"Je, hamjui kwamba miili yenu ni hekalu la Roho mtakatifu aliye ndani yenu, ambaye mlipokea kutoka kwa mungu? Ninyi basi si mali yenu wenyewe."*
Je, hujali mwili wako? Una hatia ya kutoutunza kama hekalu la Roho Mtakatifu katika tabia za kula, na mazoezi? unachafua mwili wako kwa ngono isiyo takatifu?
7. Waefeso 4:29 *"Maneno mabaya hata yasitoke vinywani mwenu."*
Je, wewe hutumia lugha chafu, hufanya mzaha usiofaa," wawaruhusu wengine kufanya hivyo ukiwapo nyumbani kwako?
8. Waefeso 4:27 *"Msimpe shetani nafasi."*
Washindwa kutambua utumiwapo na shetani kama 'uwanja wa kutua' unapomruhusu kutawala mafikira yako kupitia. Yoga, mizimu, vitabu vya mizimu, na sinema? Wapata ushauri kuhusu maisha yako ya kila siku kutokana nyota badala ya kutoka kwa Mungu? Wamruhusu shetani akutumie kupinga kazi ya Kristo kanisani mwako kwa kulaumu, udaku, kutounga mkono?
9. Waroma 12:11 *"Msilegee katika bidii, muwe wachangamfu rohoni katika kumtumikia Bwana."*
Je, wewe hucheleva kulipa madeni yako? Hukosa kuyalipa? Wanunua bidhaa zaidi ukitumia kadi za kukopa kuliko unavyoweza kulipa? Wapuuza kuweka rekodi nzuri za kodi ya mapato? Washiriki katika magendo, ukiwa mwajiri au mwajiriwa?

10. 1 Wakorinto 8:9 *“Lakini jihadharini: huu uhuru wenu usiwafanye walio na imani dhaifu waanguke katika dhambi.”*
Wajihisi waweza kufanya chochote utakacho kwa sababu Biblia husema u-huru katika Kristo? Ingawa una nguvu usiweze kuanguka, je, wewe hukosa kumsaidia mkristo mdhaifu ambaye ameanguka kwa kufuata mfano wako?
11. Waebraia 10: 25 *“Tusiache ile desturi ya kukutana pamoja.”*
Je wewe huhudhuri kanisa kama inavyotakikana? Wewe huhudhuria ibada kimwili tu, huku ukinog’oneza, ukisoma, ukifanya mipango yako wakati neno la Mungu lahubiriwa? Hukosa kuhudhuria mikutano ya sala? Umepuuza ibada za kijamaa?
12. Wakolosai 3:9 *“Msiambiane uwongo, kwani ninyi mmekwishavua ule utu wa kale pamoja na matendo yake yote.”*
Je, wewe hudanganya? Huoni kwamba uwongo mdogo mdogo ni dhambi? Husema mambo vile utakavyo yawe, badala ya vile yalivyo?
13. 1 Petero 2:11 *“Wapenzi wangu wachaneni na tamaa za kimwili zinazopigana na roho.”*
Je, wewe humwalia mwenzako wa kiume au wa kike kwa jicho la tamaa? Hujaza mawazo yako kwa vipindi vya runinga, (televisheni) sinema, vitabu na magazeti ya ngono? Mijadala yao? Kurasa zao za kati kati? Wajihusisha na vitendo vya kitamaa vinavyolaaniwa na Mungu, uasherati, usinzi, utundu?
14. Yohana 13:35 *“Mkipendana, watu wote watajua kwamba ninyi ni wanafunzi wangu.”*
Je, washiriki katika farakano kanisani mwako? Hupendelea kuchochea, kukosana badala ya kusaidia kutafuta suluhisho? Umewapenda tu watu wa kanisa lako, ukifikiri kwamba wale wa dini nyingine si sehemu ya mwili wa Yesu? Je wewe hufurahia, kisiri shida za mwingine? Unakasirishwa na ufanisi wao?
15. Wakolosai 3:13 *“Vumilianeni na kusameheana, na iwapo mmoja wenu analo jambo lo lote dhidi ya mwenzake, mnapaswa kusameheana kama Bwana anavyowasamehe ninyi.”*
Je, umekosa kumsamehe ye yote kwa chochote alichosema au kufanya dhidi yako? Umekataa kuonana na watu fulani? Una husuda?
16. Waefeso 4:28 *“Aliyekuwa akiiba, asiibe tena, bali na aanze kufanya kazi.”*
Je, wewe humwibia mwajiri wako kwa kufanya kazi kidogo kuliko inavyostahili, kufanya kazi kwa muda mfupi kuliko unavyolipwa?
17. Waefeso 5:16 *“Tumieni vizuri muda mlio nao, maana siku hizi ni mbaya.”*
Je, wapoteza wakati? Wapoteza wakati wa wengine? Watumia wakati ukitazama vipindi vya runinga (televisheni), ukisoma vitabu visivyofaa, au ukiahirisha mambo?
18. Matayo 6:24 *“Hakuna mtu awezaye kuwatumikia mabwana wawili huwezi kumtumikia Mungu pamoja na mali.”*
Je, lengo lako maishani ni kuwa na pesa nyingi iwezekanavyo? Kuchuna vitu? Umemnyima Mungu haki yake ya mapato yako. Pesa ni Mungu wako?
19. Matayo 23:28 *“Hali kadhalika nanyi mwaonekana na watu kwa nje kuwa wema, lakini kwa ndani mmejaa unafiki na uovu.”*
Je, wajua moyoni mwako kwamba wewe ni bandia anayejifunza kuwa mkristo halisi? Wajificha katika uanachama wa kanisa, kuficha maisha yaliyojaa dhambi. Wajifanya mkristo ili uheshimiwe kijamii, ukubaliwe kanisani mwako na katika jamii? Je watabasabu kumcha-Mungu wakati wa ibada za Jumapili, lakini waishi dhambini Juma zima? Je, wewe ukiwa nyumbani na wewe ukiwa nje ni mtu mmoja au wawili tofauti?
20. Wafilipi 4:8 *“Hatimaye ndungu zangu, jazeni fikira zenu kwa mambo mema na yanayostahili kusifiwa: mambo ya kweli, bora, haki, safi, ya kupendeza na ya heshima.”*
Wafurahia kusikiliza udaku? Na kueneza? Waamini udaku au ‘nusu kweli’, hasa kumhusu adui au mpinzani wako? Wakosa kusoma Biblia kila siku? Wakosa kuyafikiria mambo ya Mungu - mambo ya pekee yaliyo mazuri, ya kweli na safi?